**JINA..........................................................DARASA..................................... SAHIHI………**

**NAMBARI YA USAJILI……………………… TAREHE…………………………..**

# *MTIHANI WA MWIGO WA BUNAMFAN 2021*

# *MWONGOZO WA KUSAHIHISHA*

**Hati ya kuhitimu elimu ya sekondari**

**102/2**

**Karatasi ya 2**

**KISWAHILI ( LUGHA)**

**DISEMBA 2021**

**MUDA: SAA 2 1/2**

1. UFAHAMU

a) Kutomchapa/kumbembeleza/kumdekeza mtoto anapokosea/anapokikiuka uadilifu kunamharibu/kunamzorotesha tabia yake, au kunamfanya mtundu. (alama 2)
b) Zamani ilichikuliwa kwamba watoto na hata wanawake hawana akili lakini ukweli ni kwamba watu wote wana akili sawa, au ni utata unaoletwa na misimano miwili tofauti – wa kale na wa sasa. (alama 2)
c) Kutomwelekeza mtoto vizuri mwishowe ataharibika kama ambavyo mmea hudhoofika usipotunzwa vyema.
   - Mtoto huzorota kitabia asipopewa malezi mema.

   ( alama 4 ) (kila upande 2)

d) Watu wote wana akili sawa/Binadamu huzaliwa na akili zake hivyo basi sio haki kudharauliana kwa misingi ya kiakili/wanaume kuwadharau watoto na wanawake kuwa wana akili pungufu ni makosa. (alama 2)
e) <u>Kumwadhibu mtoto</u> kwa <u>kumnyima haki</u> zake ni <u>kuifanya akili yake isikomae</u> kikamilifu. (alama 3)
f) (i) Kulishindilia/kulifanya lieleweke/kulilazimisha/kuliingiza kwa nguvu.
   (ii) Kujiepusha/kujitia hamnazo/kujikwepa/kujipambanya/kujimbelegeza (alama 2)

**3.Ufupisho**

a)i) Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha hustawisha ufahamu wetu.

ii) Mazoezi ya kuandika hustawisha ufahamu wa kusoma.

iii) Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine.

iv) Lugha iliyoandikwa ni aina ya mazungumzo.

v) Ujuzi mwingi katika kuzungumza hupatikana shuleni.

vi) Ujuzi wa kila siku husaidia katika maendeleo ya kusoma na msamiati.

vii) Husaidia kufahamu yaliyoandikwa.

viii) Hali ya mwanafunzi (pia) ni ujuzi.
(8x1=8)

b)

i) Karibu elimu yote imeandikwa vitabuni.

ii) Lugha zote hazina ustawi sawa.

iii) Zingine hazina vitabu vingi/zina vitabu vingi.

iv) Mwanafunzi anayesoma afaa kusoma mengi kando na taaluma anayoisomea. (4x1=4)

$$M_{b4}^{a8}$$
$$u_t - {}^{3}\!/_{15}$$

**2.MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika maneno yenye sifa zifuatazo za sauti:
   **i)** Kilainishoghuna cha midomo, irabuyambele-juu, kipuaghuna cha midomo, kizuiwa ghuna na irabu ya nyuma-wastani.**(alama 1/0)**
   **wimbo**
   ii) Kikwaruzo hafifu cha ufizi, irabu ya chini-kati, kikwamizo cha mdomo-meno hafifu, irabu ya mbele-juu.**(alama 1/0)**
   **safi**

b) Tunga sentensi ukitumia nomino ya ngeli ya KU pamoja na kirai husishi cha uhusiano.
   **Kucheza kwa mtoto kutamfaidi.(alama 2/0)**
   **N RH**
   **Kulima kwa bidii kunaleta mazao.**
   **Mtahiniwa sharti atumie nomino ya kitenzijina.**

c) Ainisha uamilifu wa kisarufi wa mofimu katika kitenzi hiki.
   Kilivijisha.
   **Ki-mofimu ya ngeli**
   **li-mofimu ya wakati**
   **vi-mofimu ya watendwa/yambwa**
   **j-mzizi/shina**
   **ish-kauli tendesha**
   **a-kiishio(alama½ $\times 6 = 3$)**

d) Yakinisha kwa udogo ukitumia kiambishi cha masharti ya uwezekano.
   Mtoto asiyeiba Kitabu hajakamatwa.
   **Kitoto kingeiba kitabu kingekamatwa. (alama 2/0)**

e) Andika upya sentensi kulingana na maagizo.

Kiroboto huyo alituuma.Kiroboto aliuawa.(Tumia kivumishi kirejeshi cha kati kuunganisha.)

**Kiroboto huyo aliyetuuma jana aliuawa. (alama 1/0)**

f) Eleza matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo.
Mola ata<u>ku</u>kirimu u<u>ki</u>mtolea sadaka.
**Ku-nafsi ya pili umoja, ki-kuonyesha masharti (alama $1\times 2 = 2$)**

g) Andika upya sentensi hii kwawakati ujao hali katavu.
Mwanariadha alishiriki mbio za Tokyo.
**Mwanariadha atakuwa hashiriki mbio za Tokyo.(alama$2/0$)**

h) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate **mji** na **mchi**.
**Mji-makazi ya watu**
**Mchi-kipande maalum cha mti kinachotumika kutwangia vitu kwenye kinu.**
**Mfano**
**Mama alitwanga mchele kwa mchi akiwa kwenye mji wa Kisumu. (alama $1\times 2 = 2$)**

i) Unda kitenzi kutokana na nomino **maskani**, kisha ukitungie sentensi.
**Maskani-sakini**
**Sakini-kaamahali/fanya makazi**
**Mfano**
**Watalii wa Uingereza walisakini nchini mwetu kwa miaka miwili.**
**Tathmini jibu la mtahini.(alama $1\times 2 = 2$)**

j) Bainisha kiima nayambwa katika sentensi hii.
Omari alipewa vipuli na fundi stadi kwa bahasha.
**Fundi stadi-kiima**
**Omari-yambwa tendewa**
**Vipuli-yambwa tendwa**
**Bahasha-yambwa ala(alama$\frac{1}{2} \times 4 = 2$)**

k) Tunga sentensi kwa hali ya wastani ukitumia kihusishi cha hali.
**Vihusishi vya hali ni: kwa niaba ya, miongoni mwa, pamoja na**
**Mfano**
**Alitoa hotuba kwa niaba ya kiranja mkuu.**
**Alikuwa miongoni mwa waliopewa zawadi. (alama$2/0$)**

l) Ainisha aina za vishazi katika sentensi hii.
Marekebisho ya katiba ya BBI yatapita iwapo wananchi watahusishwa.
**Marekebisho ya katiba ya BBI yatapita-kishazihuru**
**Iwapo wananchi watahusishwa-kishazitegemezi(alama $1\times 2 = 2$)**

m) Changanua sentensi hii kwa kielelezo cha mstari.
Zohali na Zuhura ni majina yasayari.
**$S\text{-}KN_1(N+U+N) + KT(t+KN_2(N+H+N))$ (alama KN=1/0, KT-1/0)**

n) Tunga sentensi moja ya kuonyesha matumizi mawili ya vielezi vya silabi moja.
**Alipokuja tulipokuwa tulifurahia. (po ya wakati na mahali)(alama $1\times 2 = 2$)**

o) Andika kinyume cha maneno yafuatayo.
Dhahiri**-siri**
Kavu**-nyevu(alama $1\times 2 = 2$)**

p) Tambua hali katika sentensi ifuatayo.
Ukulima wa sampuli hii wasumbua wengi.
**Hali isiyodhihirika/haliya a** **(alama 1/0)**

q) Eleza maana ya msemo **shika sikio**.
**Shika sikio-jutia jambo/kupata funzo** **(alama 1/0)**

r) Tumia kibadala cha kiasi cha kuonyesha nafasi katika orodha kwenye sentensi.
**<u>Wa kwanza/wa nne/wa kumi</u> wameingia jukwaani.** **(alama 2)**

s) Andika kwa wingi sentensi hii.
Ukwato wa mnyama huyo aliufikisha ufuoni.
**Kwato za wanyama hao walizifikisha fuoni.** **(alama 2)**

t) i) Tunasemabaraza la wazee**mzengwe**wawagomajina**shuke/shazi**la nafaka.
**(alama $1\times 2 = 2$)**

ii) Audhubilahi ni tunapoapa **la hasha!/kamwe!/hata!/ata!/mawe!/la!** Tunapokana na **harambee!** tunapohimiza. **(alama $1\times 2 = 2$)**

**4.ISIMUJAMII**

a)Sajili ya kituo cha polisi

b)matumizi ya:

i)lugha ya adabu

ii)urasmi hudumishwa

iii)matumizi ya misimu

iv)kuchanganya ndimi

v)kukosa usanifu na usarufi

vi)lugha ya matusihasa kwa washukiwa wakiwa ndani ya seli

viilugha ya kuhoji

viii)lugha ya kutisha

ix)istilahi za kisheria